AckySHINE.com

# Majivuno na Kujikweza Mbele ya Mungu

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · September 4, 2020

Mafundisho ya Msingi ya Kanisa Katoliki: Makala za Katoliki · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Kutubu na Kusamehewa dhambi

Rejea Luka 14:7-24 na Luka 18 :9-18

Mungu anakawaida ya kumkweza yoyote ajishushaye na kumshusha yule ajikwezaye. Vile unavyojiona bora mbele ya Mungu na mbele ya watu ndivyo na Mungu anatakavyokuonyesha kuwa wewe sio bora au wewe sio zaidi ya wengine.

Madhara ya Kujikweza au majivuno

1. Sala zako hazitajibiwa kwa kuwa mara zote nia ya sala zako zitakua ni za kujitakia makuu. 2. Kusahau nafasi ya Mungu katika maisha yako na kuhisi unajitosheleza kwa yote. 3.Kusahau nafasi na umuhimu wa wengine kwa kuhisi kuwa hawana thamani kama wewe. Dalili za Kujikweza au majivuno

1.Kutaka au kupenda kuwa na nafasi ya kwanza kwenye kila kitu. 2. Kukosa uvumilivu 3. Kuwa na hofu ya kushindwa na kufedheheshwa 4.Kukosa upendo na kujali kwa wengine 5. Kupungua imani kwa Mungu. Yani kuhisi kama Mungu anaweza kufanya au hawezi. 6. Kupungua ukaribu wako kwa Mungu. 7.Kutokupenda kusali /kuomba Mungu. Dawa ya majivuno au jinsi ya kujishusha

1.Kujifunza unyenyekevu. 2.Kujifunza upendo wa kweli kwa Mungu na wengine. 3. Jifunze kuwaombea wengine. Hii itasaidia kujenga unyenyekevu. 4. Kujifunza kuridhika 5. Jifunze kufurahia mafanikio ya wengine. 6. Usiwe muongeaji sana na mchunguzi wa mambo ya watu sana.